



KISII UNIVERSITY

UNIVERSITY EXAMINATIONS SPECIAL/SUPPLEMENTARY EXAMINATIONS

SECONS YEAR EXAMINATION FOR THE AWARD OF THE DEGREE OF BACHELORS OF ARTS / EDUCATION SECOND SEMESTER 2024/2025 (AUGUST, 2025)

KISW 211: ISIMU JAMII

STREAM: Y2 S2

TIME: 2 HOURS

DAY: TUESDAY, 3.00 – 5.00 P M

DATE: 05/08/2025

MAAGIZO

1. Usiandike neno lolote kwenye karatasi ya maswali.
2. Jibu Maswali MATATU. Swali La Kwanza na mengine Mawili.

SWALI LA KWANZA

- a) Fasiri dhana ya Isimujamii, kisha ufafanue mambo ya msingi ambayo isimujamii hujishughulisha nayo. (Alama 12)
- b) “Isimujamii ni taaluma inayoingiliana na taaluma nyingi katika jamii.” Jadili kauli hii kwa kurejelea taaluma zozote tatu. (Alama 18)

SWALI LA PILI

Kwa kuzingatia hali ya lugha nchini Kenya, ni kwa njia gani nadharia ya Umaksi inaeleza hali hii (zingatia mvutano kati ya lugha na Kiingereza na lugha nyinginezo za Kiafrika. (Alama 20)

SWALI LA TATU

- a) “Matumizi ya lugha katika jamii hutegemea mambo mbalimbali.” Jadili kauli hii kwa kutumia mifano mwafaka na toshelevu. (alama 10)
- b) Linganisha na ulinganue mtazamo elezi na mtazamo elekezi inavyoongoza katika matumizi ya lugha. (Alama 10)

SWALI LA NNE

- a) Pambanua dhana za Pijini na Krioli, kisha uzilinganisha na kuzilinganua. (Alama 10)
- b) Jadili nadharia zozote mbili zinazoelezea asili ya pijini. (Alama 10)

SWALI LA TANO

- a) Bainisha tofauti baina ya Sera ya Lugha na Upangaji lugha (Alama 4)
- b) Dadavua hatua zozote nne ambazo upangaji wa lugha unapaswa kupitia. (Alama 16)

SWALI LA SITA

“Lugha huakisi tofauti za kijinsia katika jamii.” Fafanua kauli hii kwa kutumia mifano mwafaka (Alama 20)